JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA WA FEDHA 2020/21 KWA LUGHA RAHISI

# Toleo la Wananchi

**Imetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Policy Forum**

# 1. UTANGULIZI

## 1.1. Nini maana ya Bajeti ya Serikali Toleo la Wananchi?

Bajeti ya Serikali Toleo la Wananchi ni Kijitabu kinachoelezea mipango na bajeti ya Serikali kwa muhtasari na lugha rahisi inayoweza kueleweka kwa Mwananchi wa kawaida na wadau mbalimbali. Kijitabu hiki kinamsaidia mwananchi kuielewa na kuifahamu bajeti ya Serikali kwa mwaka husika na jinsi bajeti inavyogusa maisha ya wananchi kwa njia mbalimbali. Kijitabu hiki kinatoa fursa kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika kutoa maamuzi wakati wa mchakato wa kuandaa Mipango na Bajeti ya Serikali na hivyo kuhamasisha dhana ya uwazi na uwajibikaji katika kusimamia fedha za umma.

## 1.2. Nini maana ya Bajeti ya Serikali?

Bajeti ni mpango wa Serikali unaobainisha namna Serikali itakavyokusanya na kutumia mapato katika mwaka husika ili kutekeleza shughuli mbalimbali kwa ajili ya ustawi wa jamii. Baadhi ya shughuli ambazo hutekelezwa ni pamoja na utoaji wa huduma za kijamii katika sekta za afya, elimu, maji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

## 1.3. Mchakato wa Bajeti

Mchakato wa uandaaji wa Bajeti ya Serikali huanza kwa Wizara ya Fedha na Mipango kutoa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ambao unatoa maelekezo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu masuala muhimu ya kuzingatiwa wakati wa uandaji wa mpango na bajeti. Aidha, maandalizi ya Bajeti yamezingatia maelekezo ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21 unaobainisha vipaumbele vya Serikali na mchakato wa uandaaji wa bajeti. Hivyo, Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/21 imepitia ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwemo Baraza la Mawaziri na hatimaye kuwasilishwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Sheria ya Bajeti, Sura 439.

# 2. SERA NA MALENGO YA BAJETI

## 2.1 Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla na Bajeti

Shabaha na malengo ya uchumi jumla na bajeti kwa mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:

i. Pato Halisi la Taifa kukua kwa asilimia 5.5 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2019;
ii. Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja (kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0);
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.7 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2020/21 kutoka asilimia 14.0 mwaka 2019/20;
iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21 kutoka asilimia 12.1 mwaka 2019/20;
v. Matumizi ya Serikali kufikia asilimia 22.1 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21 kutoka asilimia 21.3 mwaka 2019/20; na
vi. Nakisi[1] ya bajeti kufikia asilimia 2.6 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2020/21.

## 2.2 Sera za Mapato

Katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali itatekeleza sera zifuatazo:

i. Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji;
ii. Kupanua wigo wa kodi na kujenga mahusiano na mazingira rafiki kwa mlipakodi;
iii. Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi;
iv. Kuimarisha usimamizi wa taasisi za umma; na
v. Kuhimiza matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mikakati ya Kuongeza Mapato:** katika kufikia malengo ya makadirio ya mapato ya ndani, mikakati ifuatayo ya kiutawala itatekelezwa:

i. Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa mashine za kutolea risiti za kielektroniki (Ukiuza toa risiti, ukinunua dai risiti);
ii. Kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji na udhibiti wa uhamishaji haramu wa fedha unaofanywa na kampuni za kimataifa kwa kuanzisha Kanzidata ya Ubadilishanaji Taarifa;
iii. Kuharakisha usambazaji wa Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG); na

---

[1]**Nakisi ya bajeti** ni tofauti kati ya mapato (ikijumuisha misaada) na matumizi katika kipindi husika.

iv. Kuwajengea uwezo Maofisa wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Pamoja na hatua za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali itaendelea kuchukua hatua ili kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

i. Kuhamasisha wananchi kushiriki katika kuwekeza kwenye Hatifungani na Dhamana za Serikali;
ii. Kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo ili kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu; na
iii. Kukopa kwa utaratibu wa udhamini kutoka taasisi za udhamini wa mikopo.

### 2.3 Sera za Matumizi

Sera za matumizi zitalenga kutekeleza hatua zifuatazo:

i. Kuendeleza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma;
ii. Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu;
iii. Kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya kuanzisha miradi mipya;
iv. Kudhibiti ulimbikizaji wa madeni; na
v. Kuongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali.

## 3. VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA 2020/21

Vipaumbele vya bajeti kwa mwaka 2020/21 vimezingatia maeneo makuu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ikiwemo: Ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; maendeleo ya watu; na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Aidha, maeneo mahsusi ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

### 3.1. Ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda:

Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo yenye matokeo makubwa katika ukuaji wa uchumi, kuzalisha ajira na kupunguza umaskini ikiwemo Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere, ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa yaani *Standard Gauge*, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na kusomesha wataalam wengi katika fani na ujuzi adimu na maalum kwa maendeleo ya viwanda na watu. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuboresha upatikanaji wa

mbegu bora, pembejeo za kilimo, kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko.




### 3.2. Maendeleo ya Watu

Maeneo mahsusi ya vipaumbele katika eneo hili ni:

i. **Maji na Usafi wa Mazingira**: kuendeleza kasi ya usambazaji maji mijini na vijijini; kusimamia vyanzo vya maji; kudhibiti ubora na kuboresha miundombinu ya uondoaji na uhifadhi wa majitaka;

ii. **Afya**: kuendeleza ujenzi wa vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa na hospitali za rufaa za mikoa; kuweka vifaa na vifaa tiba vya kisasa katika hospitali zote; na kuimarisha vituo vya mafunzo ili kuboresha ubora wa huduma katika sekta ya afya;

iii. **Elimu**: kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuendelea kugharamia elimumsingi bila ada; kuboresha utoaji wa mafunzo ya ufundi; kuimarisha ukaguzi katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya mafunzo ya ufundi na ualimu; kuongeza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia; na kuongeza fursa za upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;

iv. **Ajira na Uendelezaji wa Ujuzi**: kuongeza fursa za ajira pamoja na kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na kuhamasisha ari ya ubunifu na ujasiriamali; na


v. **Utawala Bora na Huduma kwa Umma**: kudumisha amani, ulinzi na usalama; kuimarisha mifumo na taasisi za utoaji haki; kuendeleza utawala bora na demokrasia; kupambana na rushwa; kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi; kuendelea na ujenzi wa miundombinu na

majengo ya ofisi katika Makao Makuu ya Serikali Dodoma; na kugharamia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

### 3.3. Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na:

i. Kuendelea kuwianisha kodi na tozo mbalimbali ili kuchochea biashara na uwekezaji;
ii. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya reli, barabara, nishati, viwanja vya ndege na bandari;
iii. Ununuzi na ukarabati wa meli za abiria na mizigo, na vivuko ili kuboresha huduma za usafirishaji;
iv. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa kuongeza wigo wa Mkongo wa Taifa ili kurahisisha na kuharakisha utoaji wa huduma;
v. Kuharakisha uondoaji wa mizigo bandarini; na
vi. Kuendelea kuimarisha mahusiano na sekta binafsi.




# 4. MAKADIRIO YA MAPATO YA SERIKALI

## 4.1 Vyanzo vya Mapato ya Serikali

Katika Mwaka 2020/21, Serikali imepanga kukusanya jumla ya shilingi **trilioni 34.88** kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mapato ya kodi shilingi trilioni 20.33;
ii. Mapato yasiyo ya kodi ya shilingi trilioni 2.92;
iii. Mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 815.0;
iv. Misaada na mikopo nafuu ya kibajeti shilingi bilioni 138.3;
v. Misaada na mikopo nafuu ya Miradi ya Maendeleo shilingi trilioni 2.46;
vi. Misaada na mikopo nafuu ya Mifuko ya Kisekta shilingi bilioni 275.5;
vii. Mikopo ya nje shilingi trilioni 3.03; na
viii. Mikopo ya ndani shilingi trilioni 4.90.



### 4.2 Maboresho ya Kodi, Ada na Tozo

Katika mwaka 2020/21, Serikali itafanya maboresho katika viwango vya kodi, tozo na ada mbalimbali. Baadhi ya maboresho hayo ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Sheria ya kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148

i. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bima za kilimo na mazao ili kupunguza gharama na kutoa unafuu kwa wakulima; na

**ii.** Kufanya marekebisho ya kuwawezesha wauzaji wa bidhaa ghafi nje ya nchi kuendelea kujirejeshea Kodi ya Ongezeko la Thamani iliyolipwa kwenye gharama za huduma au bidhaa katika shughuli hizo ili bidhaa hizo ziweze kushindana katika masoko ya nje.

#### 4.2.2 Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332

i. Kuongeza kiwango cha mapato ya waajiriwa yasiyotozwa kodi kutoka shilingi 170,000 kwa mwezi hadi shilingi 270,000 kwa mwezi;

ii. Kuongeza kiwango cha mapato ghafi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi yasiyotakiwa kutozwa Kodi ya Mapato kutoka shilingi milioni hamsini (50,000,000/=) hadi shilingi milioni mia moja (100,000,000/=) kwa mwaka;

iii. Kufuta msamaha wa Kodi ya Mapato kwa wazalishaji walio ndani ya maeneo maalum ya kiuchumi wanaozalisha bidhaa na kuuza ndani ya nchi kwa asilimia 100;

iv. Kutotoza kodi kwenye michango ya wadau kwenye Mfuko wa Ukimwi na michango iliyotolewa kwa Serikali;

v. Kumpa mamlaka Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato kwenye miradi ya kimkakati yenye jumla ya Kodi ya Mapato isiyozidi shilingi bilioni moja kwa kipindi chote cha mradi;

vi. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mtaji kwenye mapato yatokanayo na ubadilishaji wa leseni katika ardhi iliyohodhiwa na kupangishwa kwa mwekezaji mwingine; na

vii. Kutoza kodi ya zuio ya asilimia 10 kwenye malipo ya uwakala inayolipwa kwa mawakala wa Benki kama ilivyo kwa mawakala wa huduma za uhamishaji fedha za kieletroniki.

#### 4.2.3 Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147

i. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye bia ya unga (powdered beer) kwa kiwango cha shilingi 844 kwa kilo ya bia ya unga inayoagizwa kutoka nje ya nchi; na

ii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye juisi za unga (powdered juice) zinazotambulika kwa kiwango cha shilingi 232/= kwa kilo ya juisi ya unga

inayoagizwa kutoka nje ya nchi.

#### 4.2.4 Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290

Kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala yanayohusu Serikali za Mitaa kukusanya tozo ya huduma ya asilimia 0.3 ya mapato ghafi kwenye Sekta ya Mawasiliano kwa niaba ya Halmashauri, na kuyagawa mapato hayo kwa Halmashauri zote ndani ya siku 14 baada ya kukusanywa.

#### 4.2.5 Sheria ya Usajili wa Magari, SURA 124

Kuanzisha usajili wa magari kwa kutumia namba maalum (mfano T. 777 DDD) kwa ada ya shilingi laki tano (500,000/=).

#### 4.2.6 Sheria ya Madini, SURA 123

Kuweka vipengele vinavyomtaka mwombaji wa leseni au anayetaka kuhuisha leseni za uchimbaji madini kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (*TIN*) na cheti cha kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania.

#### 4.2.7 Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82

Kuwapunguzia waajiri kiwango cha tozo ya maendeleo ya ufundi stadi kutoka asilimia 4.5 hadi asilimia 4.

#### 4.2.8 Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya Mwaka 1999

Kuweka ulazima wa mwananchi yeyote ambaye ardhi yake imefanyiwa upimaji (survey) na michoro yake kuidhinishwa na wizara yenye dhamana ya masuala ya ardhi kupeleka maombi kwa Kamishna wa Ardhi kupatiwa Hati ya kumiliki ardhi ndani ya siku tisini (90) kuanzia tarehe ya kuidhinishwa kwa michoro ya upimaji ili kuwafanya wananchi wanaohodhi ardhi bila umiliki wafanye taratibu za kuomba umiliki.

#### 4.2.9 Ada na Tozo

Kufuta au kupunguza ada na tozo sitini (60) zinazotozwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi ili kuondoa kero, urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Marekebisho hayo yanahusisha: Tume ya Ushindani (FCC); Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Bodi ya Sukari Tanzania (SBT); Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini (OSHA); Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maliasili na Utalii; Mabango na Matangazo; Mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na sekta ya utalii.

# 5. MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI

## 5.1 Matumizi ya Serikali Katika Maeneo ya Kipaumbele


Serikali imepanga kutumia jumla ya **shilingi trilioni 34.88**, kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 22.10 (63.4%)zimeelekezwa kwenye matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 12.78 (36.6%) zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ni kama ifuatavyo:

iii. **Shilingi trilioni 8.65** kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali;
iv. **Shilingi trilioni 7.76** kwa ajili ya mishahara;
v. **Shilingi trilioni 5.21** kwa ajili ya uendeshaji wa Serikali;
vi. **Shilingi bilioni 481.9** kwa ajili ya matumizi yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri.
vii. **Shilingi trilioni 10.04** ni fedha za Maendeleo kutokana na vyanzo vya ndani
viii. **Shilingi trilioni 2.74** ni fedha za Maendeleo kutokana na vyanzo vya nje.

## 5.2 Mgawanyo wa Matumizi Kisekta

Matumizi ya Serikali yameganywa katika sekta saba (7). Mgawanyo wa bajeti katika asilimia kwa kuzingatia sekta husika ni kama ilivyobainishwa katika **Kielelezo Na. 1**

Kielelezo Na 1: Mgawanyo wa Bajeti ya Serikali Kisekta




Aidha, muhtasari wa bajeti kwa mwaka 2020/21 katika programu, miradi na shughuli mbalimbali za sekta ni kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Elimu

Katika mwaka 2020/21, Sekta ya Elimu imetengewa jumla ya **shilingi trilioni 4.72**, sawa na asilimia 13.5 ya bajeti ya Serikali. Bajeti hii imelenga kugharamia elimumsingi bila ada; mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu; kukuza ubora wa elimu na kujenga ujuzi katika ngazi zote za elimu; kuibua, kutambua, kuendeleza ubunifu na ugunduzi wa teknolojia ili kuchangia katika kuzalisha ajira. Bajeti iliyotengwa kwa baadhi ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi trilioni 3.27** kwa ajili ya uendeshaji wa elimumsingi katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo shilingi bilioni 298.13 za elimumsingi bila ada na shilingi bilioni 96.56 za uendeshaji wa mitihani ya kitaifa;
ii. **Shilingi bilioni 464.0** kugharimia mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu
iii. **Shilingi bilioni 273.41** kwa ajili ya usimamizi na udhibiti wa ubora wa elimu katika ngazi za elimu ya msingi na vyuo vya ualimu;
iv. **Shilingi bilioni 119.41** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya vyuo vikuu na maktaba za mikoa;
v. **Shilingi bilioni 105.95** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika vyuo vya ufundi;
vi. **Shilingi bilioni 86.11** kwa ajili ya kugharamia shughuli za kiutawala katika sekta ya elimu;
vii. **Shilingi bilioni 42.33** kwa ajili ya ujenzi wa maabara na vyumba vya madarasa;
viii. **Shilingi bilioni 37.91** kwa ajili ya matumizi yanayolenga kukuza ubunifu, sayansi na teknolojia na utafiti; na
ix. **Shilingi bilioni 12.70** kwa ajili ya miradi ya sayansi, teknolojia na utafiti.



Mwonekano wa ujenzo wa jengo la Chuo cha Ufundi Stadi Kasulu

### 5.2.2 Afya

Katika mwaka 2020/21, Sekta ya Afya imetengewa jumla ya **shilingi trilioni 1.92** sawa, na asilimia 5.5 ya Bajeti ya Serikali. Fedha hizo zimeelekezwa katika kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya; kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo; kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; kuendelea kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto; kuimarisha huduma za kibingwa na mafunzo kwa watumishi wa afya pamoja na kuimarisha miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi mbalimbali. Baadhi ya vipaumbele katika sekta ya afya ni kama ifuatavyo:


i. **Shilingi bilioni 543.80** kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuboresha huduma ya tiba za magonjwa mbalimbali;
ii. **Shilingi bilioni 509.53** kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya na miundombinu katika Hospital za Wilaya;
iii. **Shilingi bilioni 226.10** kwa ajili ya huduma za kinga dhidi ya maambukizi ya magonjwa mbalimbali;
iv. **Shilingi bilioni 216.06** kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya na miundombinu katika Zahanati;
v. **Shilingi bilioni 179.75** kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya na miundombinu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa;
vi. **Shilingi bilioni 172.19** kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya na miundombinu katika Vituo vya Afya;
vii. **Shilingi bilioni 55.92** kwa ajili ya shughuli za utawala na rasilimali watu katika utoaji wa huduma za afya kwenye ngazi za Mikoa na Halmashauri; na
viii. **Shilingi bilioni 12.91** kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) na kuboresha utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na VVU.




### 5.2.3 Huduma za Utawala na Deni la Serikali

Katika mwaka 2020/21, Serikali imetenga jumla ya **shilingi trilioni 13.54** kwa ajili ya kuimarisha shughuli za kiutawala ikiwemo kugharamia Deni la Serikali. Baadhi ya vipaumbele vya matumizi katika sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi trilioni 8.65** kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali;
ii. **Shilingi trilioni 1.28** kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serilikari za Mitaa;
iii. **Shilingi bilioni 388.90** kwa ajili ya ruzuku kwa kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);
iv. **Shilingi bilioni 348.49** kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa sheria na maadili ya Vyama vya Siasa; na
v. **Shilingi bilioni 180.0** kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.



### 5.2.4 Ulinzi na Usalama wa Raia

Katika mwaka 2020/21 jumla ya shilingi **trilioni 3.30** zimetengwa kwa ajili ya kugharamia matumizi mbalimbali ya sekta ya ulinzi na usalama wa raia. Baadhi ya vipaumbele na fedha zilizotengwa ni:

i. **Shilingi trilioni 2.14** kwa ajili ya shughuli za ulinzi na usalama wa nchi;
ii. **Shilingi bilioni 898.68** zimetengwa kwa ajili ya usimamizi wa sheria na ulinzi wa raia na mali zao; na
iii. **Shilingi bilioni 263.95** kwa ajili ya kusimamia upatikanaji wa haki na kupambana na utumiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.




Mwonekano wa Jengo la Mahakama ya Mwanzo na Wilaya - Kigamboni

# 6. SHUGHULI ZA UCHUMI

Katika mwaka 2020/21, sekta ya maendeleo ya uchumi imetengewa jumla ya **shilingi trilioni 8.28**. Baadhi ya vipaumbele na bajeti iliyotengwa ni kama ifuatavyo:

## 6.1 Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Katika kuchochea uwekezaji na kuongeza uzalishaji wenye tija na kipato kwa wakulima, kiasi cha **shilingi bilioni 459.74** kimetengwa kwa mchanganuo ufuatao:

i. **Shilingi bilioni 99.84** kwa ajili ya maendeleo ya mifugo na uvuvi;
ii. **Shilingi bilioni 95.0** kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya kilimo ikiwemo miundombinu ya umwagiliaji;
iii. **Shilingi bilioni 65.2** kwa ajili ya huduma za utafiti na ugani kwenye kilimo;
iv. **Shilingi bilioni 27.3** kwa ajili ya uzalishaji, upatikanaji na udhibiti wa pembejeo za kilimo, ufugaji na uvuvi;
v. **Shilingi billioni 15.0** kwa ajili ya kununua, kuhifadhi na kusambaza mazao ya

nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA); na

vi. **Shilingi bilioni 9.6** kwa ajili ya kuendeleleza na kuimarisha Vyama vya Ushirika na Ushirika.




## 6.2 Madini

Jumla ya **shilingi bilioni 62.7** zimetengwa katika sekta ndogo ya madini kwa ajili ya utekelezaji wa baadhi ya shughuli za kipaumbele kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 31.1** kwa ajili ya kuwezesha Wizara ya Madini kutoa huduma;
ii. **Shilingi bilioni 20.2** kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji wa madini;
iii. **Shilingi bilioni 6.3** kuimarisha shughuli za utafiti kwa maeneo yenye madini; na
iv. **Shilingi bilioni 4.6** kuhimiza uanzishwaji na kuimarisha masoko ya madini kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko ya madini.

## 6.3 Nishati

Katika kuongeza uwezo wa uzalishaji, usambazaji na kuunganisha umeme kwa wananchi na kutekeleza vipaumbele mbalimbali, sekta ndogo ya nishati imetengewa jumla ya **shilingi trilioni 2.20**. Fedha hizi zimeelekezwa katika shughuli za kipaumbele zikiwemo:

i. **Shilingi trilioni 1.61** kwa ajili ya miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo Bwawa la Julius Nyerere Megawati (MW) 2,115, Kinyerezi MW 185, Rusumo MW 80, Ruhudji MW 358 na Rumakali MW 80;
ii. **Shilingi bilioni 395.4** kugharamia Awamu Ya Tatu Ya Mradi wa Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA);
iii. **Shilingi bilioni 54.8** kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme

Msongo wa kilovolti (kV) 400 (Rufiji – Chalinze – Dodoma), kV 400 (Iringa - Singida – Shinyanga) na kV 400 (Singida - Arusha – Namanga); na

iv. **Shilingi bilioni 31.5** kugharamia miradi ya petroli na gesi asilia ikiwemo usambazaji wa gesi asilia viwandani; utafiti wa mafuta na gesi asilia, kuchakata na kusindika gesi asilia, kuanza biashara ya mafuta; na uimarishaji wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja.




## 6.4 Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Sekta ndogo ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetengewa jumla ya shilingi trilioni 5.16 kwa ajili ya miradi ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano ambapo fedha zilizotengwa kwa baadhi ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi trilioni 2.02** kwa ajili ya ujenzi wa Reli Ya Kati kwa Kiwango Cha Kimataifa (Standard Gauge);

ii. **Shilingi trilioni 1.40** kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuu na barabara za mikoa, ujenzi na ukarabati wa madaraja na mizani;

iii. **Shilingi bilioni 450.0** kwa ajili ya kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ikiwemo malipo ya awali ya ndege mbili (2) aina ya Boeing 787 - 8 Dreamliner na ndege moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767 – 300;

iv. **Shilingi bilioni 289.68** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Reli ya Kati kupitia Mfuko wa Reli;

v. **Shilingi bilioni 275.03** kwa ajili ya ukarabati wa barabara za mijini na vijijini

kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA);

vi. **Shilingi bilioni 148.79** kwa ajili ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa vivuko na magati;

vii. **Shilingi bilioni 91.89** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege;

viii. **Shilingi bilioni 48.16** kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Selander lililopo Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa barabara unganishi ya km 5.2;

ix. **Shilingi bilioni 39.71** kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato Dodoma; na

x. **Shilingi bilioni 3.50** kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mto Wami.



Mwonekano wa Barabara ya Juu katika Makutano ya Ubungo Jijini Dar es Salaam

## 6.5 Maliasili, Utalii na Mazingira

Katika mwaka 2020/21, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 100.33** kwa ajili ya kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili na malikale, mazingira pamoja na kuchochea maendeleo ya utalii. Baadhi ya vipaumbele na fedha zilizotengwa ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 36.2** kwa ajili ya usimamizi endelevu wa maliasili, malikale na kupambana na ujangili;

ii. **Shilingi bilioni 31.0** kwa ajili ya usimamizi endelevu wa uhifadhi wa misitu na mazingira asilia na kuongeza thamani kwa mazao ya misitu;

iii. **Shilingi bilioni 7.0** kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya ikolojia ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi; na

iv. **Shilingi bilioni 5.7** kwa ajili ya kuendeleza utalii.

### 6.6 Viwanda na Biashara

Kipaumbele kimeelekezwa katika kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda. Katika kufikia azma hii, jumla ya **shilingi bilioni 277.92** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kipaumbele zikijumuisha: utoaji wa mikopo ya mitambo na mashine kwa wajasiriamali wadogo na wakati; uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji na uendelezaji wa biashara kupitia maonesho na matangazo mbalimbali.

### 6.7 Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi

Jumla ya shilingi bilioni 21.27 zimetengwa kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi na uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia programu mbalimbali ili kuibua fursa na kukuza ajira pamoja na uendelezaji wa ujuzi. Fedha zilizotengwa kwa baadhi ya vipaumbele ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 9.26** kwa ajili ya kutekeleza programu ya kukuza ujuzi na kuongeza fursa za ajira; na
ii. **Shilingi bilioni 1.00** kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana.

## 7. HIFADHI YA JAMII

Hifadhi ya jamii kwa mwaka 2020/21 imetengewa jumla ya s**hilingi trilioni 1.85** ili kuwezesha makundi mbalimbali kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na kijamii kwa mchanganuo ufuatao:

i. **Shilingi trilioni 1.57** michango ya Serikali kwa ajili ya kulipa mafao ya kustaafu kwa watumishi na fidia kwa watumishi wanaoumia wakiwa kazini;
ii. **Shilingi bilioni 242.26** kwa ajili ya Bima ya Afya (NHIF); na
iii. **Shilingi bilioni 30.95** kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.


## 8. MAJI, MAKAZI NA MAENDELEO YA JAMII

Jumla ya **shilingi trilioni 1.27** zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za maji, makazi na maendeleo ya jamii. Mchanganuo wa bajeti katika sekta hii ni kama ifuatavyo:

### 8.1 Maji

Katika mwaka 2020/21, Sekta ndogo ya Maji imetengewa **shilingi bilioni 769.03** kwa ajili ya usambazaji wa maji pamoja na miradi ya usafi wa mazingira mijini na vijijini. Baadhi ya shughuli zitakazotekelezwa na fedha zilizotengwa ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 323.88** kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi inayoendelea na kuanza miradi mipya ya maji vijijini;
ii. **Shilingi bilioni 48.0** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji safi na usafi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam;
iii. **Shilingi bilioni 39.0** kwa ajili ya kutambua, kutunza, kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji;
iv. **Shilingi bilioni 30.21** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji mikuu, wilaya, halmashauri za miji na baadhi ya miradi ya kitaifa;
v. **Shilingi bilioni 29.2** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Same-Mwanga- Korogwe;
vi. **Shilingi bilioni 7.3** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mipya yenye kuleta matokeo makubwa kutoka kwenye vyanzo vya maji vyenye uhakika ukiwemo mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Singida hadi Dodoma; na
vii. **Shilingi bilioni 5.5** kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Tabora, Igunga na Nzega ikiwemo Miji ya Tinde na Shelui.



## 8.2 Ardhi, Nyumba na Makazi

Katika mwaka 2020/21, Serikali imepanga kutumia shilingi **bilioni 145.71** kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vikiwemo; ujenzi wa ofisi mpya za ardhi za mikoa na kuimarisha ofisi za ardhi za halmashauri, kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani na kuboresha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa njia ya kielektroniki. Bajeti iliyotengwa inalenga kutekeleza baadhi ya kazi muhimu za kimkakati zifuatazo:

i. **Shilingi bilioni 37.1** kwa ajili ya kuboresha milki za ardhi, mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi na ujenzi wa ofisi za ardhi za mikoa;
ii. **Shilingi bilioni 32.0** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani;
iii. **Shilingi bilioni 20.2** kwa ajili ya kuimarisha ofisi mpya za ardhi katika mikoa yote ili kutekeleza shughuli za upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi pamoja na usajili wa hati na nyaraka mbalimbali;
iv. **Shilingi bilioni 5.4** kwa ajili ya kuimarisha alama za mipaka ya kimataifa baina ya Tanzania na nchi inazopakana nazo; na
v. **Shilingi bilioni 1.2** kwa ajili ya upangaji miji, urasimishaji na uendelezaji makazi.




## 8.3 Maendeleo ya Jamii

Sekta ndogo ya Maendeleo ya Jamii imetengewa jumla ya shilingi **bilioni 318.62** kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma za ustawi na maendeleo ya jamii pamoja na kuongeza ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miongoni mwa maeneo ya vipaumbele na fedha zilizotengwa ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 6.6** kwa ajili ya mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii**;**
ii. **Shilingi bilioni 2.7** kwa ajili ya kujenga kumbi pacha na bweni katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru;

iii. **Shilingi milioni 827.95** kwa ajili ya programu za kutokomeza ukatili wa kijinsia katika jamii;
iv. **Shilingi milioni 700** kwa ajili ya ujenzi wa mahabusu ya watoto katika mikoa ya Kigoma na Mtwara;
v. **Shilingi milioni 400** kwa ajili ya ukarabati majengo na miundombinu katika makazi ya wazee;
vi. **Shilingi milioni 250** kwa ajili ya kuboresha Taasisi ya Ustawi wa Jamii; na
vii. **Shilingi milioni 200** kwa ajili ya kujenga Shule ya Maadilisho katika Mkoa wa Geita.



Kikao cha ushirikishwaji katika maendeleo ya jamii

### 8.4 Habari, Michezo na Utamaduni

Jumla ya **shilingi bilioni 40.14** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza sera, sheria na mipango mbalimbali katika kuendeleza na kukuza habari, utamaduni, sanaa na michezo nchini. Miongoni mwa shughuli zitakazofanyika ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 5** kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa usikivu Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC);
ii. **Shilingi bilioni 1.2** kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Vyuo vya Utamaduni na Sanaa;
iii. **Shilingi bilioni 1** ni kwa ajili ya kuboresha utoaji wa habari kwa umma; na
iv. **Shilingi milioni 515** kwa ajili ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.



Wananchi wakishiriki katika shughuli za kudumisha utamaduni



Uchukuaji wa matukio kwa ajili ya upashaji habari

## *Jedwali 1: Muhtasari wa Mgawanyo wa Bajeti Kisekta*

| Sekta | | Bajeti ya 2020/21 (bilioni) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Elimu** | | 4,721.68 | 13.54 |
| **Afya** | | 1,916.29 | 5.49 |
| **Maendeleo ya Uchumi** | Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano | 5,158.06 | 14.79 |
| | Kilimo | 459.74 | 1.32 |
| | Viwanda na Biashara | 277.93 | 0.80 |
| | Nishati | 2,196.78 | 6.30 |
| | Madini | 62.70 | 0.18 |
| | Maliasili, Utalii na Mazingira | 100.34 | 0.29 |
| | Vijana, Ajira na Uendelezaji wa Ulinzi | 21.27 | 0.06 |
| **Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii** | Maji | 769.03 | 2.20 |
| | Ardhi, Nyumba na Makazi | 145.71 | 0.42 |
| | Maendeleo ya Jamii | 318.62 | 0.91 |
| | Habari, Michezo na Utamaduni | 40.14 | 0.12 |
| **Hifadhi ya Jamii** | | 1,845.66 | 5.29 |
| **Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama** | | 3,302.71 | 9.47 |
| **Huduma za Utawala** | Huduma za Utawala (bila Deni la Serikali) | 4,893.20 | 14.03 |
| | Deni la Serikai | 8,649.94 | 24.80 |
| **Jumla** | | **34,879.79** | **100** |

**NYARAKA REJEA ZA BAJETI**

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka rejea za Serikali zilizotumika kuandaa Kijitabu cha Bajeti Toleo la Mwananchi kwa mwaka 2020/21:

1. Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025;
2. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21;
3. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020;
4. Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati ya mwaka 2020/21;
5. Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2020/21;
6. Hotuba za Bajeti za Wizara za Mwaka wa Fedha 2020/21;
7. Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2020/21;
8. Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020;
9. Sheria ya Matumizi ya Mwaka 2020;
10. Sheria ya Bajeti 2015, Sura 439; na
11. Vitabu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 (Juzuu Na. I, II, III na IV).

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo yaliyotangulia ya Vitabu vya Bajeti ya Serikali Toleo la Mwanachi, unaweza kutembelea tovuti ya:

- Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz)
- Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

## Kwa maelezo zaidi kuhusu Bajeti ya Serikali

Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- Nyaraka zenye taarifa za Bajeti ya Serikali (***angalia orodha ya nyaraka za rejea***) hususan, nakala ngumu ya Vitabu vya Bajeti ya Serikali ambavyo vinapatikana Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 2802, Dodoma.

- Nakala laini za Vitabu vya Bajeti ya Serikali vinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango http://www.mof.go.tz

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na Bajeti ya Serikali. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.

**Kwa maoni yako jaza ukurasa huu na kutuma Wizara ya Fedha na Mipango**

Toa maoni yako kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/21

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, unahitaji ufafanuzi zaidi ya uliotolewa katika kijitabu hiki?

□NDIYO □HAPANA

Kama jibu ni NDIYO Je, unahitaji ufafanuzi katika eneo gani?

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, ni kwa kiasi gani kijitabu hiki kimekusaidia?

□ Kiasi kikubwa □ Wastani □ Hakikunisaidia

Je, ni kwa kiasi gani kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka?

□ Rahisi □ Wastani □ Ngumu

Tuma maoni yako katika anuani ifuatayo

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Fedha na Mipango,**
**Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali,**
**Mtaa wa Hazina,**
**Mji wa Serikali – Mtumba,**
**40468 Dodoma,**
**Sanduku la Barua 2802,**
**DODOMA-TANZANIA**

Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa:
**ps@hazina.go.tz**